

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

**MKOA WA IRINGA**

Simu Na: 026 - 2702264

Fax: 026 - 2702264

Barua pepe:iringarrh@afya.go.tz

moi@iringarrh.go.tz

**Unapojibu tafadhali taja:**



Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,

Mtaa wa Kinondoni,

S. L. P. 260

**IRINGA**

**Kumb.Na.** IRRH/L.10/1/Vol.II/73

25 Aprili, 2024

**TANGAZO LA KAZI YA MKATABA YA KUJITOLEA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi kwa Mkataba wa kujitolea, katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa kwa nafasi 05 za Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja II kama ifuatavyo:-

**1. Afisa Muuguzi Msaidizi II – Nafasi 05**

**(a) Sifa za Mwombaji**

Awe na Stashahada (Diploma) ya Uuguzi ya muda usiopungua miaka miwili(2) kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Ukunga Tanzania.

**(b) Kazi na Majukumu**

- (i) Kutoa huduma za Uuguzi
- (ii) Kukusanya takwimu muhimu za Afya
- (iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
- (iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- (v) Kutoa huduma za kinga na uzazi
- (vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, ujuzi na uzoefu wake

**Sifa za Jumla za Waombaji**

- a) Awe Raia na Tanzania
- b) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- c) Awe na cheti cha ufaulu cha kidato cha nne(IV)

- d) Awe na cheti cha ufaulu cha taalumu husika na usajili wa baraza la Uuguzi nia Ukunga(TNMC)
- e) Awe na leseni ya uuguzi iliyo hai(Valid Licence)
- f) Ambatanisha cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho(NIDA)
- g) Uwasilishaji wa Taarifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria
- (i) Waombaji watakaokidha vigezo wataitwa kwenye usaili

### **MSHAHARA**

Waombaji watakaofaulu usaili watapewa Mkataba wa miezi mitatu mitatu na watalipwa kulingana na makubaliano na Mwajiri.


Maombi yote yaambatanishwe;:-

1. Barua ya Mwombaji
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa na Nida
3. Nakala ya cheti cha kidato cha Nne
4. Nakala ya Vyeti vya Taaluma(Cheti na Transcript), Wasifu(CV), na Leseni ya Uuguzi(TNMC)
5. Picha ndogo (Passport size) mbili za hivi karibuni

Barua zote za maombi yawasilishwe/yatumwe kwa njia POSTA au fika Ofisi ya Masjala ya Wazi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 Mchana (Jumatatu - Ijumaa) Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe **05.05.2024** saa **9:30 Mchana**. Hatutapokea maombi kwa njia ya barua pepe.

Maombi yatumwe kwa:-

Mganga Mfawidhi,  
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,  
S. L. P. 260,  
**IRINGA**

  
Dkt. Scholastica Malangalila  
Kaimu Mganga Mfawidhi  
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa  
**IRINGA**